OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(OR-TAMISEMI)
HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA

Shule ya Sekondari ya Mazoezi Klerruu,
S.L.P 2531,
IRINGA.
04/12/2020

Simu : 026-2701098- MEZANI
Simu : 0752507519 (Mkuu wa Shule)

KUMB. NA. KLERCU/S/40/1

Kwa Mzazi/Mlezi wa
…….....

YAH: MASHARTI YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA MAZOEZI YA KLERRUU MWAKA 2021.

Awali ya yote ninachukua fursa hii kukupongeza kwa kufaulu mtihani wako wa darasa VII, kitendo ambacho kimekuwezesha kuchaguliwa na kujiunga na kidato cha kwanza.

Ni matumaini yangu kwamba nafasi hii utaitumia vizuri kukuwezesha kufanikisha katika masomo na shughuli nyingine za shule kama vile uzalishaji mali, michezo n.k.

Aidha, ni tegemeo langu pia kuwa utakuwa na nidhamu nzuri na utatekeleza na kufuata sheria na kanuni zote za shule hii pamoja na masharti yote ya kujiunga kama yalivyo orodheshwa hapo chini.

Shule ya Sekondari ya Mazoezi ya Klerruu ni shule ya kutwa na ni ya mchanganyiko.

Shule itafunguliwa tarehe **11/ 01/2021**Mzazi/mlezi, unatakiwa kufika tarehe 0**7/1/2021** na mtoto wako ili ufanye mambo yafuatayo:

(a)Ujaze fomu ya ahadi ya mzazi

(b) Ujaze fomu ya uandikishaji

(c)Ukabidhi fomu ya kupimwa afya na nakala ya cheti cha kuzaliwa.

(d) Mtoto kufahamu mazingira ya shule.

Ninakukaribisha wewe mwanafunzi na Mzazi/Mlezi hapa shuleni kwa mashauriano kuhusu ufanisi wa kazi yetu. Ninakutakia maadalizi mema kwa kutimiza maagizo kama ifuatavyo:

VIFAA VYA KULETA SHULENI

(a)Madaftari 9 makubwa na kalamu za kuandikia (pens and pencils)

(b) Mkebe wa vifaa vya hisabati (mathematical set).

(c)Mfuko/begi la kubebea madaftari

(d) Sahani na kijiko kwaajili ya chakula cha mchana ambacho wazazi mnakichangia na kukisimamia

Utakaguliwa unaporipo shuleni.

SARE ZA SHULE- WASICHANA.

(a) Blauzi mbili (2) nyeupe tetron **mikono mifupi**

(b) Sketi 2 za shule ndefu rangi ya kijani zinazofunika mguu wote zenye marinda madogo,**urefu kutokachini kwenye unyayo iwe ni inchi 6**

(c) Jozi mbili za viatu **vyeusi vya ngozi visivyo na kisigino kirefu vya kufunga kwa gidamu.**

(d) Jozi mbili za soksi nyeupe ndefu.

(e) Sweta la rangi ya bluu lililofumwa lenye umbo la “V” mbele.

(f) Nguo za michezo, raba jozi moja, bukta na sketi- Vitakaguliwa siku ya kuripoti.

(g) Mwanfunzi anahitajika kuwa na nywele fupi zisizotiwa madawa wala kusukwa.

(h) Makoti, majaketi na masweta ya rangi nyingine **hayaruhusiwi.** hereni, mikufu/ shanga, simu, bangili, n.k haviruhusiwi kuvaliwa au kuja navyo shuleni.

(i) Vazi lingine lolote nje ya sare za shule iwe ni soksi, viatu,sketi,sweta, n.k likivaliwa shuleni, hatua za kinidhamu

zitachukuliwa dhidi ya mwanafunzi mhusika, ikiwa ni pamoja na kuharibiwa kabisa kwa vitu hivyo.

SARE ZA SHULE –WAVULANA

(a) Shati mbili (2) Nyeupe tetroni **mikono mifupi**

(b) Suruari mbili za shule ndefu rangi ya kijani kilichoiva zinazotosha vizuri**. Suruali zinazobana na fupi(modo) haziruhusiwi. Ikumbukwe kuwa sare ya shule haina fasheni.**

(c) Jozi mbili za viatu vya ngozi nyeusi **visivyo na kisigino kirefu vya kufunga kwa gidamu**

(d) Jozi mbili za soksi rangi yoyote.

(e) Sweta la rangi ya bluu lililofumwa lenye umbo la "V" mbele.

(f) Nguo za michezo raba jozi moja na bukta

(g) Mwanafunzi anahitajika kuwa na nywele fupi zisizotiwa madawa

(h) Makoti na majaketi hayaruhusiwi. Vazi lingine lolote nje, ya sare za shule iwe soksi, viatu, suruari, n.k vikivaliwa shuleni, ni kukiuka taratibu za shule, kwa hiyo hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya mwanafunzi mhusika, ikiwa ni pamoja na kuharibiwa kabisa kwa vitu hivyo.

MAMBO YA KUZINGATIA

(a) Kumbuka kwamba mwanafunzi anatakiwa awe ameripoti shuleni si zaidi ya siku 21, kama kuna sababu za msingi baada ya shule kufungua.

(b) Mwanfunzi anaposhindwa kufika shule kutokana na ugonjwa au tatizo lolote, mzazi/ mlezi atoe taarifa kwa mkuu wa shule siku hiyo hiyo, vinginevyo atahesabiwa kuwa mtoro

(c) Kila siku mwanafunzi akisharipoti shuleni haruhusiwi kuondoka bila ruhusa maalumu ya mwalimu –kwa kupewa kibali au fomu ya ruhusa**.**

(d) Mwanafunzi akifika shuleni baada ya saa moja asubuhi atarudishwa nyumbani

(e) Mwanafunzi asipofika shuleni kwa muda wa siku 30 atasimamishwa shule.

(f) Ni matumaini ya uongozi wa shule kwamba , mzazi/mezi ataitwa shuleni kwa mashauriano

iwapo itabidi kufanya hivyo, mzazi asipoitikia wito, mtoto atarudishwa nyumbani

(g) Ni matumaini ya uongozi wa shule kwamba, mzazi/mlezi atakuwa karibu na walimu katika

kufuatilia **MAHUDHURIO, MAENDELEO, TABIA NA MWENENDO WA**

MWANAFUNZI.

(h) Iwapo mzazi/ mlezi atabadili anuani ni muhimu mzazi/mlezi mwenyewe aujulishe uongozi wa shule kwa kuambatanisha uthibitisho maalumu ili iwe rahisi kufanya mawasiliano. Aidha iwapo mwanafunzi atalazimika kuhama shule, lazima mzazi/mlezi(**sio mwanafunzi**) atoe maelezo yenye kuthibitisha sababu za uhamisho huo.

(i) Kila mwanafunzi awapo hapo shuleni ni lazima ahudhurie vipindi vyote na shughuli zote za nje . Mwanafunzi akikosa vipindi 10 asilimia 25 ya vipindi vyote kwa mwezi bila sababu

zinazokubalika atarudishwa nyumbani.

(j) Kila mzazi/ mlezi hakikisha unafuatilia ripoti ya maendeleo ya mwanafunzi kila muhula. Kwa hiyo mzazi/ mlezi utalazimika kufika wewe mwenyewe mara tu zinapokuwa tayari shuleni. Kila mwisho wa muhula mzazi/ mlezi ahakikishe ripoti anaipata na kufika shuleni kwa majadiliano kama itabidi. Kwa mfano watoto walio na wastani chini ya alama **45** katika mitihani yetu **lazima waje na wazazi shule inapofungua kuja kufanya mazungumzo na walimu ya namna ya kumsaidia mtoto.**

NB: IFAHAMIKE WAZI KUWA UENDESHAJI NA MAFANIKIO YA SHULE UNATEGEMEA ZAIDI USHIRIKIANO UNAOKUWEPO KATI YA WALIMU, WAZAZI NA WANAFUNZI.

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule hii kama zilivyo shule zote nchini ina msimamo wa maadili mema. Sheria na kanuni za shule zinazingatia vipengele vifuatavyo:

1.HESHIMA

Katika kusisitiza heshima shuleni mambo yafuatayo yazingatiwe:

(i)Wanafunzi wanatakiwa kusimama na kumsalimia mwalimu au mtu yoyote anayewazidi umri wanapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.

(ii)Wanafunzi hawaruhusiwi kutumia lugha mbaya wakati wowote kati yao wenyewe, kwa walimu wao na kwa watu wengine.

(iii) Wanafunzi wanatakiwa kuwaheshimu wafanyakazi wote waliyoko shuleni kwao kama walezi wao.

(iv)Wanafunzi wanatakiwa kusaidiana na kushirikiana katika kazi.

(v)Wanafunzi wanatakiwa kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote.

(vi) Wanafunzi hawaruhusiwi kufanya mambo yafuatayo

(a) kuvuta sigara

(b) kufuga kucha ndefu na kuwa na nywele zisizowekwa katika hali ya usafi

(c) kufuga ndevu

(d) kuvaa mavazi yasiyo ya heshima

(e) kugombana

(vii) Wanafunzi wanatakiwa kuitika mara moja na kukimbia wanapoitwa.

(viii) Wanafunzi wanatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa na fedha za serikali,

nembo ya Taifa (coat of Arms) na wimbo wa Taifa.

(ix) Wanafunzi wanatakiwa kuheshimu ukumbi wa mikutano, ofisi za shule, mali binafsi na mali ya umma.

(x)Wanafunzi wanatakiwa kunyoosha mkono juu na kusimama wanapojibu na kuuliza maswali

(xi) Wanafunzi wanatakiwa kusimama katika mistari wakati wa kupokea huduma na matangazo.

(xii)Wanafunzi wanatakiwa kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia njema popote walipo.

(xiii)Wanafunzi wanatakiwa kukaa kimya wakati wote wanapokuwa darasani, wassitoke nje bila ruhusa yamwalimu au kiongozi aliyopo.

1. **MAHUDHURIO**

(i) Wanafunzi wanatakiwa kuhudhuria shule kwa muda wote wa masomo.

(ii) Wanafunzi wanatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.

(iii) Wanafunzi wote wanatakiwa kufanya kazi zote za mikono zinazotolewa shuleni.

(iv) Wanafunzi wote wanatakiwa kuhudhuria mikutano ya shule kama baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya Taifa mikutano ya darasa nk.

TANIBIHI(MUHIMU)

Ili kuhakikisha kuwa mahudhurio ni kamilifu utaratibu wa kuita majina (rollcall na classjournal**)**utazingatiwa

2. **KUWAHI**

(i) Wanafunzi wanatakiwa kujua, kuzoea na kuthamini muda

(ii) Wanafunzi wanatakiwa kuwahi katika shughuli zote za shule zilivyopangwa katika ratiba kila siku, wachelewaji watachukuliwa hatua za kinidhamu.

(iii) Wanafunzi wanatakiwa kuwahi wanaposikia wito wa dharura.

(iv) Kutakuwa na kengele itakayowajulisha wanafunzi muda wanaotakiwa kwa shughuli mbalimbali.

3. **SARE YA SHULE**

(i) Shule inayo sare inayojulikana kwa wanafunzi na jumuiya nzima na ipo katika mshono unaokubalika na kulingana na heshima inayosisitizwa kitaifa.

(ii) Uvaaji wa sare ya shule unasisitizwa kwa wanafunzi wakati wote wa;

(a)Masomo darasani

(b) Wanafunzi wanapotoka nje ya shule kwa shughuli za kishule.
(c)Mhadhara wa shule (school baraza)
(d) Wanafunzi wanaposafiri kutoka nyumbani kwenda shuleni na kurudi nyumbani.

(iii) Shule inasisitiza umuhimu wa wanafunzi kuwa na nguo za michezo na wazitumie wakati wa michezo tu.
(iv) Usafi wa sare na mavazi yote yaliyoruhusiwa kuvaliwa shuleni unasisitizwa na utakaguliwa.
(v) Kofia na mapambo mengine yoyote haviruhusiwi kuvaliwa pamoja na sare.

4. MIPAKA YA SHULE

(i) Shule inayo mipaka inayofahamika kwa jumuiya yote.
(ii) Wanafunzi hawaruhusiwi kutoka nje ya mipaka hiyo isipokuwa kwa kibali maalumu.
(iii) Shule inatoa fomu ya ruhusa ya kutoka nje ya mipaka ya shule kama kuna umuhimu huo.
(iv) Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalumu;
(a)Chumba cha mwalimu
(b) Ofisi za walimu
(c) Maabara
(d) Majumba ya kufikia wageni na majumba ya starehe
(e)Vilabu vya pombe nk.

5. USAFI

Usafi wa mwili na mazingira kwa wanafunzi ni sehemu muhimu ya maisha yao ya kila siku.

6. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

(i) Wizi
(ii) Uasherati, ubakaji ushoga na usagaji
(iii) Ulevi na matumizi mabaya ya madawa ya kulevya.
(iv) Uvutaji bangi
(v) Makosa ya jinai
(vi) Kupiga na kupigana
(vii) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
(viii) Kudharau bendera ya Taifa, nembo na alama za Taifa.
(ix) Kuoa au kuolewa
(x) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
(xi) Kutoa mimba
(xii) Kugoma, kuchochea na kuvuruga Amani na usalama shuleni.
(xiii) Kukataa adhabu kwa makusudi.

TANBIHI: YAPO MAKOSA MWANAFUNZI AKIYAFANYA ATAJAZISHWA FOMU MARA TATU MBELE YA MZAZI WAKE KABLA YA HATUA KUCHUKULIWA. HII NI KATIKA KUDHIBITI UWEZEKANA WA TABIA MBAYA KUSAMBAA SHULENI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Shule ya Sekondari Klerruu,
S.L.P 2531,
IRINGA.

A: YAH: MWANAFUNZI KUKUBALI NAFASI YA SHULE NA MASHARTI YA KUJIUNGA.

Mimi……(mwanafunzi) nimesoma kwa makini barua na masharti ya kujiunga pamoja na sheria/ kanuni za Shule ya Sekondari ya Mazoezi Klerruu. Kwa heshima na unyenyekevu ninaikubali/ ninaikataa nafasi hiyo kwa sababu
……
……. ninayakubali/nayakataa masharti/sheria za shule kwa sababu
…….....
……
……
Sahihi
Tarehe

B: YAH: MZAZI /MLEZI KUKUBALI NAFASI YA SHULE NA MASHARTI YA KUJIUNGA.

Mimi …….. Mzazi /mlezi wa ……..
Ambaye amechaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari ya Mazoezi Klerruu nimesoma masharti ya kujiunga pamoja na sheria/kanuni*
Ninaikubali/ninaikataa nafasi hiyo.
Ninaahidi kumtimizia kijana wangu maagizo yote ya kujiunga na shule hiyo katika muda uliopangwa.

Nitashirikiana na uongozi/jumuia ya shule katika kumkuza na kumlea mwanangu.

Asante,
Jina la Mzazi/Mlezi ……
Anwani ……..
Kitongoji/Mtaa ninaoishi…….
Namba ya simu: Nyumbani…….
Ofisini…… Mkononi……

Sahihi ……
Tarehe……

*Futa lisilohusika
Mzazi akibadilisha anwani au kuhama, atujulishe mara moja anwani mpya.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(OR-TAMISEMI)
HALMASHAURI
SHULE YA SEKONDARI YA MAZOEZI KLERRUU
FOMU YA KUPOKELEWA SHULENI.

1. Jina kamili la mwanafunzi……
   ……
2. Mahali ulipozaliwa
   ……
   …..
3. Tarehe ya kuzaliwa……
   ……
4. Anwani ya nyumbani……
   …….
5. Anwani ya Mzazi (kama ni tofauti na hiyo hapo juu)…….
6. Jina la Mzazi/Mlezi……
   …….
7. Kazi yake……
   ……
8. Ndugu wa karibu:

S/NA.	JINA	UHUSIANO	NA. YA SIMU	ANWANI YAKE	MTAA ANAOISHI
i					
ii					
iii					
iv					

9. Dini/ Madhehebu……..
10. Kidato anachoingia……
11. Shule ya msingi uliyotoka…….
12. Shule ya msingi uliyomaliza darasa la saba (kama tofauti na ya juu)……..
13. Shughuli unazopendelea mbali na masomo kama mpira wa miguu mpira wa mikono, riadha, kuimba n.k ……
14. Wilaya unakotoka…… Mtaa…….. Kata…….
15. Wilaya unayoishi …….. Mtaa…… Kata……..
16. Mjumbe wa shina/Balozi…… Mwenyekiti wa mtaa…….
17. Je wazazi wa mwanafunzi ni watanzania? Ndiyo/ Hapana. Ulete cheti cha kuzaliwa.

Sahihi ya Mwanafunzi……

Tarehe……

Matumizi ya Ofisi:

Namba ya shule……..

Namba ya mtihani wa darasa la saba……

Shule ya Msingi uliyosoma …….

Ulete chati cha kuzaliwa

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

FROM THE HEAD OF SCHOOL
KLERRUU PRACTISING SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 2531
IRINGA

TO: MEDICAL OFFICER
GOVERNMENT HOSPITAL

Full name of student……..Age……. Sex……

Please examine the above named student, with regard to his/ her physical and mental fitness for attending a full time secondary education school.
To be completed by medical officer in respect of all entrants;
Blood count (red and white)
……..
Urine
analysis……
Syphilis test
……..
Eye
test…….
T.B
Test……
Ears
……
Chest
……
.
Spleen
……
Abdomen
……

ADDITIONAL INFORMATION: egg physical or chronic family diseases e.t.c
……
……
……
……..
I certify that the above is fit/ unfit for pursuing his/ her studies

Signature……..
Designation …….
Section ……....
Date …….

Students must bring completed form when they come to report to school. No student shall be admitted for enrolment without the certificate of physical and mental fitness.

……..
HEAD OF SCHOOL
KLERRUU PRACTICING SECONDARY SCHOOL